KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO UNIONI YA KUSINI MWA TANZANIA

CHAMA CHA WACHUNGAJI/HUDUMA ZA MAOMBI

SIKU 100 ZA MAOMBI: MACHI 27 – JULAI 04, 2020

MADA: KUMWITA YESU KATIKA HITAJI LETU LA HARAKA

Limeandaliwa na Melony Coleman – Mke wa Mchungaji kule Oregon

Mtafsiri: Mch. Herbert I. Nziku – Mratibu - Huduma za Maombi: STUM

Mei 01 – 07, 2020

MALAIKA PANDE ZOTE

Inanipasa kuwashirikisha uzoefu wa ajabu nilioupitia hivi karibuni.

Mume wangu ni mchungaji katika jimbo la Oregon nchini Marekani na ulikuwa ni usiku wa ufunguzi wa mikutano yetu ya injili ya, "Ufunuo wa Matumaini." Nimekuwa nikihimiza maombi zaidi katika kanisa letu, kwa hiyo niliamua kuwa msimamizi wa chumba cha maombi wakati wa mikutano. Timu yangu inajumuisha zaidi marafiki wazee wanaokaa nyumbani au watu wanaoomba kutokea majumbani mwao, kwa hiyo nilikuwa sina hakika ni wahusika kiasi gani ningekuwa nao wakati wa mikutano. Niliamua kuanzisha chumba cha maombi hiyo hivyo, nikitumaini kwamba baadhi ya washiriki wa kanisa wangetamani kuja kuomba kwa vipindi mbali mbali wakati wa mikutano.

Usiku wa Ijumaa ya kwanza nilikuwa pekee yangu. Nilijisikia upweke, lakini niliomba hivyo hivyo. Sabato jioni tena, nilikuwa mimi tu. Kidogo lilijisikia kukatishwa tamaa. Niliweka wimbo mzuri wa "Sala ya Bwana." Ulipokuwa unapiga nilikuwa naomba. "Ninajua kwamba walipo wawili au watatu wamekusanyika kwa jina lako, unakuwepo pale Bwana. Lakini vipi kama nipo peke yangu?" Niliomba kimya kimya.

Wimbo ulipoisha, nilifungua macho yangu na chumba kilikuwa kimejaa malaika. Nilianza kulia nikitazama kuzunguka chumba kwa mshangao. Malaika walikuwa warefu, warefu hadi darini, wakiwa mabega mapana. Walisimama wakiwa wamebanana na migongo yao ikiwa ukutani, kuzunguka miisho ya chumba. Nilijiona mdogo nikijilinganisha nao. Walikuwa na mabawa na walivaa nguo kama makanzu ya kurukia. Nilivutwa kutazama nyuso zao. Walikuwa kama wanaume, wanaume watanashati. Macho yao yalikuwa ya wema sana na walitabasamu kwa upole, tabasamu yenye kufariji. Maumbile ya nyuso zao yalikuwa wazi na walizungukwa na hali ya ushupavu kama wa makamanda wa vita. Nywele zao nyeusi ziliangukia mbegani mwao. Mwonekano wao uling'aa ukiwa na rangi ya njano na nyeupe. Niliweza kuwaona kwa muda wa sekunde nne hadi tano na kisha walitoweka, lakini sikuacha kulia jioni ile yote.

Nilikuwa nimekatishwa tamaa sana, nikijiuliza ikiwa Mungu angetenda iwapo ningekuwa mimi peke yangu ndani ya chumba cha maombi. Alinionesha kwa njia ya muujiza kwamba endapo mtu mmoja anaomba, inatosha. Ninajiona duni na nisiyestahili kupewa kipawa hiki. Mara nyingi huwa nalia ninapofikiria juu ya uzoefu huu mtakatifu.

Ninaendelea kuomba ndani ya chumba cha maombi cha kanisa letu nikiwa pekee yangu, lakini sijakata tamaa tena, kwani najua kuwa chumba kimejaa malaika hata kama siwaoni. Ilinipasa kuwashirikisha! Hatutakiwi kupuuza nguvu ya maombi. Hata kama ni mtu mmoja anayeomba, inatosha. Mungu yupo kazini hata wakati ambapo sisi hatuoni.

Maswali ya Moyoni: Je! Kuna wakati unajisikia mpweke kwenye maombi? Je! Umewahi kuomba na kuomba tena na bado hukuona majibu uliyoyasubiri? Au Je! Umekuwa ukijiuliza italeta tofauti gani kwani unaomba peke yako? Kama unajaribiwa kukata tamaa, kumbuka kuwa Yesu alikuwa akiomba peke yake na tazama ambavyo maombi yake yalivyoubadilisha ulimwengu! Wafikirie Ibrahimu, Yakobo, Yusufu, Daudi, Elia, Esta, na wengine wengi katika

karne zote. Wakati fulani walijisikia kuwa wako peke yao, na bado maombi yao yaligusa mbingu.

Changamoto Hai ya Moyoni: Juma hili tunakupatia changamoto, chagua mmoja au wawili kati ya wahusika wa Biblia waliotajwa hapo juu, na ujifunze yote uwezayo kuhusiana na muda wao wa maombi wakiwa peke yao. Unapojifunza na kufanya utafiti wako tumia Biblia na Roho ya Unabii, na uandike mambo uliyoyangundua. Kisha chagua jambo moja unalolikubali toka katika nyanja moja ya maisha yao ya maombi, na uombe Mungu aipandikize hiyo roho ya maombi ndani yako.

"Ilikuwa ni kwa sababu Eliya alikuwa mtu wa imani kuu ndio maana Mungu aliweza kumtumia katika zahama ile kubwa katika historia ya Israeli. Alipokuwa anaomba, imani yake ilizifikia na kuzishika ahadi za Mbinguni, na alidumu katika sala hadi maombi yake yalipokuwa yamejibiwa. Hakusubiria kupata uthibitisho kamili kwamba Mungu alimsikia, bali alitamani kujihatarisha kupitia dalili hata ndogo sana za kibali cha Mungu. Na bado kile alichowezeshwa kufanya chini ya Mungu, wote wanaweza kufanya katika maeneo ya shughuli zao katika huduma ya Mungu... Imani kama hii inahitajika leo ulimwenguni – imani itakayoshikilia ahadi za neno la Mungu na kukataa kuziachilia hadi Mbingu itakapojibu." (Prayer, p. 138)

Mapendekezo ya aya za ziada za kusoma juma hili

- Ellen White, *The Truth About Angels***.**
- Cindy Mercer, *Pray Big: God Can Do So Much More!*

Siku ya 36, Ijumaa, Mei 1, 2020

Sifa: Tunamsifu Mungu kwa ajili ya vikundi vyote na huduma za kanisa kwa kuendelea kutafuta njia za kiubunifu na zenye msaada za kuwafikia wale wanaoshindwa! Maisha ya watu wengi yanaguswa na Yesu.

MAMBO YA KUOMBEA

- Ombea washiriki wa kanisa wanaoishi kwenye miji yenye watu wengi ulimwenguni kote wakati huu wa hili janga. Ombea ulinzi wao na upatikanaji wa mahitaji yao.
- Ombea uvumilivu miongoni mwa wataalamu wa afya ulimwenguni kote ambao wamekuwa wakipambana na janga la coronavirus kwa majuma na miezi sasa.
- Ombea watu wa Mungu ili waendelee kujifunza neno lake kwa kina, kutumia muda kwa maombi, kuacha dhambi zao, na kujiandaa kwa kuja kwa Yesu.
- Mwombe Mungu akuoneshe namna ya kuomba katika wakati huu wa janga.

Siku ya 37, Jumamosi, mei 02, 2020

IMANI CHINI YA JARIBIO

“Tazama, mimi ni Bwana, Mungu wa wote wenye mwili; je! Kuna neno gumu lo lote nisiloliweza?” Yeremia 32:27

“Mungu atapima, kwa kiwango cha juu, imani na ujasiri wa wale ambao ameweka kwao dhamana ya wajibu katika kazi yake. Kila mara mionekano itakuwa dhaifu. Ingawa Mungu amerudia rudia kutoa uhakikisho wa msaada wake, bado imani huwa kama yenye kusita. ‘ndivyo asemavyo Bwana,’linatakiwa kuwa ndilo tegemeo letu imara, bila kutegemea mantiki za kibinadamu, au mazingira ya mambo yasiyowezekana.” (Sign of the Times, June 30, 1881).

Maswali ya Moyoni: Kwa vile tunajua kwamba majaribu makubwa na majaribio yapo mbele siku za usoni, tunawezaje kukuza imani isiyotikisika itakayokuwa imara hata chihi ya jaribio? Zingatia kisa cha marafiki watatu wa Danieli waliokabiliana na tanuru la moto (soma Danieli 3). Unadhani ni kitu gani kilichowaandaa kusimama imara katika ile siku ngumu?

Sifa: wakati huu ambapo watu wengi inawapasa kukaa majumbani taarifa zinakuja za namna Mungu anavyofungua fursa za kushangaza kwa ajili ya Uinjilisti kwa njia ya mtandao na njia za kushuhudia. Mwinjilisti Robert Costa ameandaa mikutano ya uinjilisti kwa njia ya mtandao na watu 245,000 walikuwa wakifuatilia mkutano wa hivi karibuni kwa njia ya mtandao. Mwinjilisti John Bradshaw ndio amenza mikutano na makumi elfu wanahudhuria kwa njia ya mtandao.

MAMBO YA KUOMBEA

- Ombea wataalamu wa afya walioko mstari wa mbele wanaoendelea kupambana na hili janga. Ombea usalama wao wa kiafya dhidi ya COVID-19.
- Ombea wanasiasa wenye kufanya maamuzi wajue wakati salama wa kuzifungua tena nchi zilizo kwenye mazuio. Ombea njia yenye uwiano yenye kuzingatia usalama wa raia kiafya na uchumia wao.
- Omba kwa ajili ya taasisi nyingi, na biashara ndogo zinazopambana na upungufu wa kifedha kama matokeo ya kufungiwa ndani. Omba watu waweze kutafuta njia za kuzinusuru biashara ndogo ndogo zisifungwe moja kwa moja.
- Ombea wanawake na watoto walio katika hali ya hatari na wanaohitaji msaada. Omba kwa ajili ya njia za kuwafikia wenye mazingira magumu na walio dhaifu katika jamii yako.
- Omba kwa ajili ya wale wanaofanya kazi kwenye mabenki, maduka, vituo vya mafuta, na biashara zingine muhimu. Omba kwamba walindwe wasipate Coronavirus wanapoendelea kushughulika na watu wengi wanaowaendea kwa ajili ya huduma.

Siku ya 38, Jumapili, Mei 03, 2020

KUTOKA KUTOWEZEKANA HADI KUWEZEKANA

“Yesu akawakazia macho, akasema, Kwa wanadamu haiwezekani, bali kwa Mungu sivyo; maana yote yawezekana kwa Mungu.” (Marko 10:27)

“Mambo ya asili yasiyowezekana hayawezi kuzuia utendaji wake Anayeweza yote.” (DA, p. 535)

“Tunaye Mungu ambaye sikio lake halijafungwa kwa ajili ya maombezi yetu; na iwapo tutalithibitisha neno lake, ataiheshimu imani yetu. Anatutaka sisi tuwe na mapenzi yetu yote yakiwa yamefumwa pamoja na mapenzi yake, ndipo anaweza kutubariki kwa usalama; kwani ndipo hatutachukua utukufu nafsini mwetu wakati baraka ni zetu, bali sifa zote tutampa Mungu. (RH, June 9, 1891)

Maswali ya Moyoni: Mara nyingi imani yetu kwa Mungu ni ndogo kwa sababu hatutambui kwa uhalisia ukuu wa Mungu wetu. Tunadhani kwamba matatizo yetu ni makubwa kiasi kwamba hawezi kuyatatua. Tunasahau kwamba tunamtumikia Mungu aliyezitandaza mbingu kwa uweza wake mkuu na hakuna jambo lililogumu sana kwake. Leo, tumia muda kutafakari juu ya ukuu wa Mungu. Orodhesha tabia na sifa alizonazo Mungu peke yake. Unapofanya shughuli hiyo rahisi, mwombe Mungu aongeze ufahamu wako na uelewa wa yeye hasa alivyo.

Sifa: Tunamsifu Bwana kwa sababu wengi wa watu wa Mungu wanadhihirisha imani katika uongozi wake na wanatafuta milango iliyo wazi ya fursa badala ya kulenga tu kwenye milango ambayo yawezekana imefungwa wakati wa hili janga.

MAMBO YA KUOMBEA

- Omba kwamba kuhusiana na hali hii ya zahama watu waweze kumwuliza Mungu kwamba – “Je! Mungu anajaribu kutwambia kitu fulani?” (1 sam. 3:10)
- Ombea watu wengi kwenye nchi masikini wasio na kazi na wanaoshindwa kupata hata chakula cha msingi kama vile mchele na unga wa mahindi. Wengi wako kwenye hatari ya ukosefu wa chakula.
- Ombea mioyo ya watu ifunguke ulimwenguni kote ili waweze kutoa na kusaidia, na pia waombee walio kwenye zahama (Mithali 22:9, Zaburi 86:6-7)
- Ombea wakulima wanaohangaika katika kupanda na kuvuna mazao na wafanyakazi wanaowasaidia wawe salamma.

Siku ya 39, Jumatatu, Mei 04, 2020

UWEZA WA KIMBUNGU

“Sasa najua kuwa Bwana amwokoa masihi wake; Atamjibu kutoka mbingu zake takatifu. Hawa wanataja magari na hawa farasi, Bali sisi tutalitaja jina la Bwana, Mungu wetu.” (Zaburi 20:6, 7)

“Watashindana na nguvu za ushirikina, lakini wamehakikishiwa msaada usio wa kawaida. Wenye akili wote wa mbinguni wamo kwenye hili jeshi. Katika safu za vyeo wamo zaidi ya malaika. Roho Mtakatifu, mwakilishi wa kapteni wa jeshi la Bwana, hushuka kuongoza pambano. Udhaifu wetu waweza kuwa mwingi, dhambi na makosa yetu yaweza kuwa ya kuhuzunisha; lakini neema ya Mungu ni kwa wote wanaoitafuta kwa toba. Nguvu ya Mungu mwenye uweza wote imechukua nafasi badala ya wale wanaomtumainia Mungu. (DA, p. 352)

Maswali ya Moyoni: Je! Wakati fulani huwa unatamani kuona jeshi la malaika likiizunguka nyumba yako, maisha yako, na familia yako? Tafakari kisa cha Elisha na kile kilichotokea Mungu alipoyafumbua macho ya mtumishi wake (soma 2 Wafalme 6:17). Fikiria namna hofu ya mtumishi wake ilivyobadilishwa kuwa imani alipoona magari ya moto. Ni visa gani vingine kwenye biblia unavyoweza kutafakari ambapo Mungu alifumbua macho ya wanaume na wanawake ili waone malaika?

Sifa: Tunamsifu Mungu kwani watu wa Mungu wengi wanakuwa waaminifu katika kurudisha zaka na sadaka na baadhi hata wanapanga kutoa zaidi kwa sababu ya upungufu unaoweza kujitokeza kwa sababu ya wengi kuwa nje ya kazi.

MAMBO YA KUOMBEA

- Ombea wanaofanya kazi za usalama, kama vile maofisa wa polisi na wengine. Kadiri ukosefu wa usalama wa kiraia unavyozidi kuongezeka katika baadhi ya maeneo duniani, omba ulinzi kwa ajili ya wanaume na wanawake hawa.

- Ombea viongozi wa serikali wafanye kazi kwa umoja badala ya kudhoofishana wao kwa wao kwa manufaa ya kisiasa.

- Ombea matibabu na kinga zitakazo punguza au kuzuia janga hili kwa haraka zaidi ya wanavyotabiri wataalamu.

- Ombea makanisa mahalia yawe na umoja, uamsho wa kiroho na kuweka umuhimu zaidi kwenye utume. Tunapokea mahitaji mengi toka ulimwenguni kote kwa ajili ya masuala haya.

Siku ya 40, Jumanne, Mei 05, 2020

KUAMINI PASIPO KUONA

“Yesu akamwambia, Wewe, kwa kuwa umeniona, umesadiki; wa heri wale wasioona, wakasadiki.” (Yohana 20:29)

“Imani humpokea Mungu katika Neno lake, pamoja na hisia au pasipo hisia. Ni hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana. Tunaweza kuwaamini wanadamu wenzetu, Je! Hatuwezi kulitumainia Neno la Mungu? Tunapomwendea ili kupata hekima na neema, haitupasi kujitazama wenyewe kuona kama ametupatia hisia maalum kama uthibitisho kwamba ametimiza neno lake. Hisia sio kigezo.Wakristo wanapotegemea hisia kumekuwa na matokeo ya uovu mkuu. Nitajuaje kuwa Yesu anasikia maombi yangu? – Ninajua kupitia ahadi yake. Anasema atawasikia wahitaji wanapomlilia, na ninaliamini neno lake. Hajawahi kumwambia, ‘mbegu ya Yakobo, unitafute bure.’ Ikiwa tutatembea katika nuru, tunaweza kukikaribia kiti cha rehema kwa ujasiri mtakatifu. Tunaweza kuwasilisha ahadi za Mungu kwa imani iliyo hai, na kusisitiza maombi yetu. Ingawa sisi tu dhaiffu, na wenye makosa, tusiostahili, ‘roho hutusaidia katika udhaifu wetu’...Tunapokuwa tumepeleka maombi yetu mara moja, haitupasi kuacha, bali tuseme, kama alivyofanya Yakobo aliposhindana na malaika, ‘sikuachi, usiponibariki’ na kama yeye (Yakobo) tutashinda. (Echo, September 24, 1894)

Maswali ya Moyoni: Ni jambo moja kuamini wakati muujiza ukiwa mbele yako, wakati unapoweza kuona kwa macho yako. Lakini, vipi kuhusu nyakati ambapo hatuoni majibu, hatuoni miujiza, hatuwaoni malaika, na hatuoni wema wa Mungu katika maisha yetu?Je! tutaendelea kumtumaini Mungu kwa uaminifi hata wakati hatuelewi? Unapotafakari maswali haya, soma Waebrania 11:1, Warumi 8:24-25, Marko 9:24, Ayubu 13:15.

Sifa: Tumshukuru Mungu kwani katika sehemu nyingi idadi ya watu wenye maambukizi mapya ya COVID-19 inapungua.

MAMBO YA KUOMBEA

- Omba kwamba mataifa na uchumi utakapokuwa unafunguliwa kusiwepo kujirudia kwa ongezeko la idadi ya watu wanaopata maambukizi.

- Tuombee Huduma kwa Wachina katika Jiji la Cebu, kule Ufilipino na Indonesia kwa ajili ya ulinzi dhidi ya coronavirus na kwa watu wengi wa China katika kila nchi wawe na hamasa zaidi ya kumtafuta Yesu na kweli za Bibilia

- Omba kwamba taifa la China lenye watu bilioni 1.4 lifunguliwe zaidi kwa ajili ya kuenea kwa injili.

- Omba kwamba tuweze kuutumia muda wa ziada tulionao nyumbani kwa ajili ya kijifunza Biblia kwa kina na kuwafundisha watoto wetu namna ya kujifunza na kulipenda Neno la Mungu.

Siku ya 41, Jumatano, Mei 06, 2020

KUTOKA MAHALI PA SIRI

“Lakini tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu. Pande zote twadhikika, bali hatusongwi; twaona shaka, bali hatukati tamaa; twaudhiwa, bali hatuachwi; twatupwa chini, bali hatuangamizwi; siku zote twachukua katika mwili kuuawa kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu.” (2 Kor. 4:7-10)

“Kutoka mahali pa siri pa maombi ilitoka nguvu iliyoutikisha ulimwengu katika Matengenezo Makuu. Pale, watumishi wa Bwana, wakiwa na utulivu mtakatifu, walikita miguu yao juu ya mwamba wa ahadi zake. Wakati wa pambano kule Augusburg, Martin Luther ‘hakupitisha siku bila kutumia angalau saa tatu katika maombi, na zilikuwa ni saa zilizochaguliwa kutoka kwenye zile saa zinazofaa zaidi kwa kujifunza.’ Kwenye upweke wa chumba chake alisikika akimimina roho yake mbele za Mungu kwa maneno, ‘yaliyojaa ibada, kicho, na tumaini, kama mtu anapoongea na rafiki.’ ‘Ninajua kuwa wewe ni Baba yetu na Mungu wetu, alisema, ‘na kwamba utawatawanya watesi wa watoto wako; kwani wewe mwenyewe uko hatarini pamoja nasi. Jambo hili lote ni lako, na ni katika kigingi chako tu, ndipo tulipoweka mikono yetu. Kwa hiyo, tutetee, Ee Baba!” (GC, 210)

Maswali ya Moyoni: Ni kitu gani unachokitamani zaidi? Ni nini kilio cha kina cha moyo wako? Yawezekana ulikuwa hujalifikiria hili hivi karibuni. Inawezekana unajaribu kujikimu. Au yawezekana unalifikiria hilo kila wakati. Tumia muda fulani leo kufikiria kuhusu ni wapi tunaweza kupata furaha yetu kuu na hali ya kuridhika Na unapofanya hivyo tafakari Zaburi 27:4, na umwombe Bwana akupatie moyo wenye njaa ya kweli ya kuwa katika uwepo wake.

Sifa: Msifu Mungu kwamba washiriki wa Kiadventista na makanisa yao wamekuwa wakimwomba Mungu kwa ajili ya njia za kiubunifu za kuzifikia jamii zao zinazowazunguka. Na kwamba Mungu anajibu maombi haya kwa kuruhusu njia nyingi za kiubunifu.

MAMBO YA KUOMBEA

- Ombea wazee, watoto, na watu walio katika hatari miongoni mwetu.
- Ombea washiriki wa kanisa wanaojifunza namna ya kujenga urafiki na Waislamu
- Ombea hekima ya namna ya kuwaongoza kwenye ukweli wakimbizi ambao hivi karibuni wamehamishwa kutoka kwenye maeneo yao.
- Ombea makanisa ulimwenguni kote yawe na imani na kuanzisha vituo vya mvuto katika miji iliyokaribu nao.
- Ombea umwagwaji wa Mvua ya Masika kwa kanisa, kazi iweze kumalizika ili twende nyumbani.

Siku ya 42, Alhamisi, Mei 07, 2020

AMANI KAMILI

“Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea Katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini. Mtumainini Bwana siku zote Maana Bwana YEHOVA ni mwamba wa milele.” (Isaya 26:3-4)

“Wale wanaompokea Yesu kupitia Neno lake, na kuzisalimisha roho zao katika ulinzi wake, maisha yao kwenye utaratibu wake, watapata amani na utulivu….Hakuna jambo la ulimwengu linaloweza kuwahuzunisha wakati Yesu akiwafanya wawe na furaha kwa uwepo wake ” (DA, p. 331)

Maswali ya Moyoni: Unapokosa amani moyoni mwako, unakimbilia wapi kwanza? Unamwuliza nani? Ni Yesu? Kuweka matumaini yetu kwa Yesu, Mwamba wetu wa Milele, hakuwezi kutegemea namna unavyojisikia katika wakati wo wote mahsusi. Ni lazima uchague kumtumainia, bila kujali hali uliyomo. Ndipo anapoweza kukupatia amani kamili. Je! Unachagua kuweka tumaini lako kwake sasa?

Sifa: Kupitia mikutano mbalimbali kwa njia ya mtandao pamoja na shughuli zingine za kanisa kuwafikia watu kidijitali, washiriki wa zamani na waliokuwa hawajulikani waliko, wamepata hamu ya kumtafuta Mungu na hata kujiunga na kanisa tena!

MAMBO YA KUOMBEA

- Ombea washiriki wa kanisa wanaojifunza namna ya kushiriki tumaini lao pamoja na watu wa mataifa wa kisasa wanaoishi katika majiji ya ulimwengu, kwa njia inayowafaa.
- Ombea watendakazi watakaotumia njia ya Kristo kukidhi mahitaji na kuifikia mioyo ya watu wanaoishi mijini ulimwenguni kote.
- Ombea wale walio katikati ya janga la COVID-19, wanaoumwa wao wenyewe, au wapendwa wao wanahangaika na ugonjwa.
- Ombea amani kwa ajili ya washiriki wa kanisa ulimwenguni kote wenge hofu na waoga, au wanaojisikia upweke.